



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO
YA UFUNDI STADI



MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 01 mwezi 02 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha VETA-MARA, S.L.P. 188,
MUSOMA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya
Ufundi Stadi, S.L.P. 802 DODOMA (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama
“Mwajiri”) kwa upande mmoja;

NA

AMOSI CHACHA RYوبا S.L.P. 114, MUGUMU
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama “Fundi”) kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya
BULIAMA;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali
za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya
BULIAMA;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya
PLUMBING FINISHING - ADMIN, KITCHEN & DINNING, HOSTELS &
CONSTRUCTION OF CONCRETE HAND WASHING BASIN (KITCHEN & HOSTEL)

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na
Mchanganuo wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi
itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 1,950,000, kwa maneno MILION MOJA LAKI TISA NA ELFU HAMSINI Fundi atafanya kazi ya PLUMBING FINISHING kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80: 30% ya Gharama ya Ufundi;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi; na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio": 5% ya Gharama ya Ufundi.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 01/2/22 mwezi 02 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.
- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 30 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.
- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

- (a) Kujenga PLUMBING FINISHING na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaavya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA VETA-MARA.

Jina: DAVID L. BENEDICT Saini: _____

Wadhifa: MWAMAMIZI WA MRADI BUTIAMA DVIC Tarehe: _____

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ALFRED G KIDIFU Saini: _____

Wadhifa: AFISA MANUNUZI Tarehe: _____

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: AMOSI CHACHA RYOKA Saini: _____

Wadhifa: FUNDI Tarehe: _____

Mbele ya (Shahidi)

Jina: EDWARD MAREGESI Saini: _____

Wadhifa: SHAHIDI Tarehe: _____

VATIC MANAGER
P.O. BOX 188
MUSOMA - MARA
01/02/2022

LOGISTICS OFFICER
VATIC
P.O. BOX 188
MUSOMA - MARA
01/02/2022

01/02/2022

01/02/2022